


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



Tarehe: 18.08.2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro inawatangazia wananchi wote ndani ya Halmashauri ya Ngorongoro kuwa kuna nafasi ya wazi ya **Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira** ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa kipindi cha miaka mitano.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe Raia wa Tanzania na mwenye akili timamu, mstaafu katika Utumishi wa Umma mwenye umri wa kati ya miaka **55** hadi **65**
- Awe mwadilifu
- Awe na ujuzi na utaalumu katika moja ya fani zifuatazo:-
  - Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resource Management)
  - Utawala wa Umma (Public Administration)
  - Sheria (Law).

**MALIPO**

Kazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira haina malipo. Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atalipwa posho ya vikao vya bodi kadiri vikao vitakavyojitokeza au kadiri atakavyohudhuria vikao kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Serikali.

**MAELEZO YA JUMLA**

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:-

- Cheti cha kuzaliwa
- Nakala za vyeti vya Elimu/Taaluma (Certified)
- Barua ya utambulisho toka kwa mwenyekiti wa Serikali ya kijiji ikiwa na picha ndogo tatu za hivi karibuni.
- Wasifu binafsi (CV).

2. Barua toka kwa wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili.

3. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **01.09.2022** saa **9:30 Alasiri**.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro,  
**55 Barabara ya Mkapa,**  
**23782 ORGOSOROK, NGORONGORO.**

Tangazo limetolewa na:-

  
Dkt. Jumaa Mohamed Mhina  
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
NGORONGORO.**



*Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*